# MOCHIWA: MWANARIKA NA RAFIKI

*Y. I. Rubanza*

Tumekutana mara ya kwanza Chuo cha Ualimu Korogwe Januari 1967 – sote tukiwa na umri wa miaka 19. Mochiwa alizaliwa Machi 1946 mimi nimezaliwa mwezi Juni 1946. Baada ya miaka miwili Mochiwa alipangwa kufundisha mkoa wa Ruvuma – mimi Kigoma. Miaka minne baadaye tukakutana Dar es Salaam na kuendeleza taaluma, yeye akinitangulia mwaka mmoja Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mwaka 1978 tukawa darasa moja la Mahiri wa Isimu na Lugha.

Miaka miwili baadaye tukawa pamoja tena tukiwa walimu wa Idara ya Kiswahili tulikaa ofisi moja. Tulifundisha Idara moja hadi mwaka 2006, alipostaafu na kujiunga na Chuo Kikuu Huria, lakini tuliendelea na harakati za pamoja za kuendeleza Kiswahili.

- **Sifa zake za kitaaluma ni pamoja na:**

| | |
|---|---|
| > Bachela wa Sanaa (Ualimu) | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 1977 |
| > Mahiri wa Sanaa (Isimu) | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 1979 |
| > Mahiri wa Sanaa (Isimu) | Chuo Kikuu cha Illinois, Urbana Champaign 1986 |
| > Daktari wa Falsafa (Isimu) | Chuo Kikuu cha Illinois, Urbana Champaign 1988 |

**1. Mochiwa – Mwalimu na Mwanataaluma**

- Mwalimu wa shule za msingi 1969 – Juni 73
- Mwendelezaji lugha (BAKITA), Wizara ya Utamaduni na Vijana
- Mwanataaluma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – Mhadhiri Msaidizi – Profesa Mshiriki (1980 – 2006).
- Profesa Mshiriki – Chuo Kikuu Huria cha Tanzania 2006 – 2008
- Mtafiti/Mwandishi wa:

| | |
|---|---|
| - Vitabu | 3 |
| - Monografi | 2 |
| - Sura katika vitabu | 3 |
| - Makala zilizochapishwa (Isimu na Lugha) | 19 |
| - Makala nyinginezo | 7 |

**3. Mochiwa – Mpambanaji na Mpiganiaji Kiswahili**

3.1 Muendelezaji lugha - Wizara ya Utamaduni na Vijana 1.7.79 – 31.1.80

3.2 Mtafiti wa lugha - BAKITA 1.7.73-30.6.74 na 1.4.77 - 30.6.78

3.3 Ufundishaji wa Lugha ya Kiswahili

(a) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Taasisi zake:

- Sintaksia, Semantaki, Pragmatiki, Isimu Jamii
- Mihadhara Idara ya Kiswahili/Isimu na Lugha za Kigeni

(b) Vyuo na Taasisi nyinginezo:

- Taasisi ya Uandishi wa Habari
- *International School of Tanganyika*
- Chuo Kikuu cha Illinois, Marekani
- Chuo Kikuu cha Bergen, Norway

- Mshiriki katika mradi wa Lugha za Tanzania uliofadhiliwa na SIDA/SAREC.
- Mfasiri wa makala mbali mbali za Taasisi kama vile Kuleana, ILO, UNDP, na Mjumbe wa UNESCO.

3.4 Mshiriki katika shughuli za uendelezaji wa Kiswahili Taasisi ya Elimu

- Kuandaa vitabu – Shule za Msingi na Sekondari
- Kuhariri vitabu
- Kufundisha walimu kazini
- Kuhudhuria/kuendesha warsha, makongamano, mikutano, mara nyingi akiwa Mwenyekiti
- Kushiriki katika warsha za msamiati/istilahi.

3.5 Mochiwa – Redio/Televisheni

Kushiriki katika vipindi maalumu vya uendelezaji wa Kiswahili

- Ngano za ushairi
- Mtu chake
- Lugha ya Taifa
- Mbinu za Kiswahili
- Ulimwengu wa Kiswahili

3.6 Ametunga na kusahihisha mitihani ya kidato cha IV na cha VI (Baraza la Mitihani)

3.7 Mjumbe wa Kamati ya Utendaji wa Chama cha Washairi.

3.8 Mtetezi wa Kiswahili kutajwa katika Katiba ya Nchi kuwa Lugha ya Taifa 2004-2008.

4. **Mochiwa – Mtendaji makini/Kiongozi shupavu**
   - Licha ya ufundishaji (hasa masomo magumu) ya Kiswahili – Msimamizi wa wanafunzi wa shahada za uzamili na uzamivu.
   - Mwenyekiti wa Semina, Warsha, na Kongamano
   - Mwalimu wa wanafunzi wageni wasomao Kiswahili
   - Mratibu wa shahada ya Uzamili, Isimu na Lugha
   - Mjumbe wa Baraza la Kiswahili (BAKITA) mara kadhaa tangu mwaka 1973
   - Mjumbe wa Kamati mbalimbali za BAKITA
   - Mwenyekiti BAKITA kuanzia tarehe 14 Mei, 2003 hadi 13 Mei 2006
   - Mjumbe wa Kamati ya Siasa – Tawi la Bwawani Kijitonyama, mwalikwa katika vikao vya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM.

5. **Mochiwa – Muumini mahiri na kiongozi wa dini.**
   - Mwaka 1999 (Desemba) amepata upadri na kuwa padri wa kanisa la Anglikana la Sindeni
   - Amejenga makanisa mawili: moja Sindeni na jingine Kwamchagga
   - Hadi anakutwa na mauti alikuwa Padri wa kanisa la Mtakatifu Albano Upanga.

6. **Mochiwa : Mtu wa watu**
   - Katika ufundishaji na ushauri wa wanafunzi amewasisitizia wanafunzi kugundua vipaji vyao na kuwaongoza ili wavivuke.
   - Mwadilifu, mchangamshaji wa mazungumzo, mpole na mtaratibu.
   - Hakupenda makuu; watu wengi wa kawaida hawakumjua kuwa ni mtu mwenye shahada na profesa licha ya kuwa kiongozi wa dini

**Baadhi ya kazi za Prof. Mochiwa**

***MAKALA***

1. "Kiswahili: The Defining Feature of Democracy in Tanzania." Katika Kimambo (ed) *Humanities and Social Sciences in East and Central Africa: Theory and Practice.* 2003.
2. 'Verbs of Wide Combinatory Possibilities: The Case of PIGA" katika *Kiswahili Jz.62* TUKI 1999.
3. 'Elimu au Maigizo? Uhakiki wa Sera ya Lugha katika Elimu Tanzania' (*Kioo cha Lugha-*) 2000.

4. 'Subtractive Multilingualism: An Educational Legacy in Tanzania?' (FLL Journal) 2000.
5. "Utotoni hadi Ungumbaru: Matatizo ya Elimu Tanzania' in *Kiswahili katika Elimu*, Z.N. Tumbo-Masabo et. Al. (eds). TUKI 1999.
6. "Uambajengo wa Viulizi katika Kiswahili," in *Kioo cha Lugha* Juzuu 1 Na. 1
7. "Bifocalism or Unifocalism in Education? A Critical Evaluation of Language Policy in Tanzania?" in *Issues in Language and Education* (ILE), Boston University African Studies Center. 1991.
8. "Mofolojia ya Kiswahili" A Chapter of a Secondary School Swahili Course Book bearing the title *Kiswahili Sekondari* Published by the Institute of Curriculum Development. 1988.
9. "Tafsiri ya Matangazo" Lugha Yetu 17 Julai, 1983.
10. "Kiswahili Sanifu: Fasili na Vidokezo vyake" *Mulika* 18, 1986
11. "Utumizi wa Kiswahili" *Lugha Yetu* 31 Desemba, 1980
12. "Dhamira za Kijiji chetu" *Mulika* 14, 1978/1976
13. "Hatia ya hatia" *Mulika* 8 Septemba, 1976
14. "Hekima ya Ushari: Rangi Zetu" *Lugha Yetu* 22 Oktoba, 1974
15. "Fasihi katika Jamii" *Lugha Yetu* 22 Oktoba, 1974
16. "Hekima ya Ushauri Kifo" *Lugha Yetu* 20 Aprili, 1974.
17. "Matamshi na Maandishi ya Kiswahili" *Lugha Yetu* 19 Januari, 1974
18. "Methali Zetu" *Lugha Yetu* 13th Oktoba, 1973
19. "Matatizo ya Tahjia za Kiswahili", *Lugha Yetu* 17 Julai, 1973.

***VITABU***

1. *Mwanasimba Hali Mbara.* Hadithi ya Watoto. Educational Publishers and Distributors Ltd 1995.
2. Poetry: *Mvumilivu Hula Mbovu.* Mkusanyo wa Mashairi. Dar es Salaam University Press. 1988.
3. *Kizigula: Msamiati wa Kizigula-Kiswahili-Kiingereza.* LOT, Chuo Kikuu Dar es Salaam, 2008.

## *MAKALA/MISWADA AMBAYO HAIJACHAPISHWA*

1. "Depletion as both a Syntactic and Semantic Phenomenon: The Case of Swahili" Dissertation in Partial Fulfilment of the requirements for Ph.D. (1988) – Illinois, Urbana – Champaign.
2. "The Problems of Teaching the Swahili Verbs *Kuwa* and *Kuwa na* to English Speaking Students' ((Makala ya Muhula, Chuo Kikuu cha Illinois) 1986.
3. "The Problem of Teaching Yes-No Questions to English Speaking Students" (Makala ya Muhula, Chuo Kikuu cha Illinois) 1986.
4. "Kizigua Tonology: A Preliminary Survey" (Makala ya Muhula, Chuo Kikuu cha Illinois) 1985
5. "Matumizi ya Register katika Magazeti", Makala yaliyowasilishwa kwenye Semina ya Waandishi wa Habari iliyoandaliwa na UNESCO, Dar es Salaam, Juni 1982.
6. "The impact of Kiswahili on Other Ethnic Languages: The Case of Handeni." District, (1979), Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Hayajachapishwa).
7. "Mikakati ya Utekelezaji wa Sera ya Kiswahili kwa Kufundishia." -- Yatachapishwa na BAKITA/Idara ya Kiswahili.